Mafundisho ya kosi hii

Je nini mafundisho ya Biblia ya Habari Njema

Huduma ya kiuinjilisti

Unaweza kumtabmbulisha Yesu kwa marafiki zako na ndugu zako kupitia kwa kikundicha Habari Njema. Tunajifunza kutoka kwa historia ya Kanisa kwamba vikundi vidogo vidogo kila mara vinakuwa njia ya kufikia watu wapya.

Huduma ya walei

Kam mtu mlei au ambaye si mwana theologia anahitaji maandalizi mengi. Kikundi hiki ni rahisi sana kupanga. Kadri unavyokuwa na vikundi vingi katika kanisa lako ndivyo wakristo wa kawaida anashiriki katika uinjisti.

Kujinfunza kwa kugundua

Kwa sababu washiriki wanajibu maswali, kila mara nyingi wanagundua mambo mengi juu ya somo. Watu huwa wanajifunza kikamilifu kwa kugundua wenyewe badala ya kusikia yale watu wengine wamegundua tayari.

Sehemu ya kukutana na Yesu

Yesu nidye neno lilifanyika mwili, inamaana tunaweza kukutana naye katika neno la Biblia. Shabaha ya Masomo ba Biblia ya habari njema si kufundisha maneno ya msingi ya Ukristo, ila kuwacha watu wakutane na mwokozi aliye hai. Yesu mwenye anakutana na washiriki wakati wa kipindi masomo ya Biblia, kuwafariji na kuwazaidia . Tazama Math.18:20.

Ni ushirika ambao hata wasio Wakarito wamekaribishwa

Tunapojadili mistari ya Biblia, kitu kinafanyika kwetu pia. Roho zinafunguliwa; washiriki hushirikishana matatizo yao wao kwa wao pamoja na Yesu pia. Na ushirikiano ukiwa na maana, watu huleta marafiki zao na hapo kikundi kunaanza kukuwa.

Je kuna tofauti gani kati ya Masomo ya kawaida ya Biblia na kikundi cha Habari njema?

Bila shaka kikundi cha masomo ya Biblia washiriki huwa wana ufahamu kuhusu Ukristo. Haipo hivyo katika Masomo ya Biblia ya Habari Njema – maswali yameandikwa kwa njia ambayo hata watu wapya wanaweza kushirikia katika majadiliano. Washiriki wanaongozwa ili waweze kutumia mistari katika maisha yao kwa msaada wa maswali. Kitu kingine zaidi: katika vikundi vya Habari Njema hawapo tu kwa minajili ya ”majibu sahihi” lakini kuwatia moyo washiriki kusema yale wanaamini na kumaanisha.

Tuanze na kutia moyo

Kutia moyo kwa mfanya kazi wa Kanisa

Wafanyi kazi wa Kanisa lazima waamini kuwa wakristo wa kawaida hujifunza Masomo ya Biblia ya Habari Njema kwa kikundi kuliko wenyewe. Pia tunajifunza kutokana na makosa yetu. Ni kama kukuza watoto: unaweza kufanya yote vema na kwa haraka kuliko mtoto wako, lakini ukifanya yote mwenyewe yeye hawezi soma chochote. Kwa miezi michache Paulo alicha Kanisa mikononi mwa Wakristo, k.m. " Basi, sasa nawaweka katika mikono ya Mungu, na kwa neno la neema yake, ambalo laweza kuwajenga na kuwapa urithi pamoja nao wote waliotakaswa " (MDO 20:32). Kwa nini inachukua mda mrefu kwa wakati wetu? Pia, tunaweza kusoma kutoka historia ya Kanisa kuwa katika kipindi cha uamsho vikundi vidogo vidogo wakristo wa kawaida waliongoza. Amin Roho Mtakatifu! Si wewe wala kiognozi wa kikundi cha Masomo ya Biblia ya Habari Njema ambaye anaweza kuifanya Masomo ya habari Njema kuwa hai; Yes utu na Roho wake Mtakatifu.

Motisha ya Wakristo

Wambie wahsarika wako kuwa kuna Baraka kila mara kwa wale ambao wanafungua milangu ya nyumba zao kwa mkusanyinko unaozingira Biblia. Usianze kikundi cha Habari Njema katika nyumba kubwa, chukua na nafasi kutoka ukutma huu hadi ule kukiwa na chakula kizuri mwishowe. Kama ukifanya, ukifanya hivyo itakuwa vigumu kuanziasha vikundi vingine katika nyumba zao. Utahitaji kuanza katika nyumba za kawaida ili wengine wafuate. Ambia Usharika wako kuwa kikundi cha Habari Njema kinaweza kuzaidia kanisa lako kwa njia tatu:

1. Wanaleta watu wapya katika ibada na katika batizo.
2. Vinazaidia wakristo wa zamani kukua Kiroho.
3. Wanalea viongozi wapya.

Jinsi ya kuchagua viongizi wa kwanza wa kikundi

Usiulize watu ambao wana kazi nyingi na mambo mengi. Usiulize watu ambao ni wazungumzaji na wanatawala katika mazungumzo. Uliza wale ambao waliongoka juzi, au wale ambao binfsi wametiwa moyo na Masomo ya Biblia ya Habari Njema..

Usiange na nadharia, anza na uzoefu

Ni muhimu kuelewa kwamba shabaha ya vikundi vya Habari Njema bila kujiuzisha na Masomo ya Biblia ya kawaida. Unweza kuuliza watu wazoefu waje kanisani mwako ili waweze kuongoza hapo Masomo ya Biblia ya Habari Njema. (tazama ukrasa wa mwisho.) Halafu unaweza kutimia maswali ya Habari Njema katika mikutano mingi, kempi n.k. hadi Wakarisot wote wa Kanisa lako wameshiriki katika Masomo ya Biblia kwa njia hii.

Kikundi

Je inawezekana kubadilisha kikundi cha zamani kuwa cha Habari Njema?

Inawezekana lakini sio rahisi. Kadri kikundi kilivyo cha zamani na washiriki wake kadiri ilivyo vigumu kubadilisha. Badala ya kujaribu kubadilisha cha zamani, anza kikundi kipya.

Uanze lini?

Baada ya mikutano ya kiroho ni mda mzuri wa kuanza, pia unahitaji kushauri watu wageni ambao wanakuja katika Ibada za kila Jumapili na mikutano mingine waweze kuingia katika mikutano ya kikundi cha Habari Njema Habari Njema.

Ukubwa wa kikundi watu kati ya 4-8.

Kama Wakristo wawili wakiwaalika marafiki zao wawili, tayari una kikundi cha watu wane. Kikundi kikizidi watu 8 lazima kugawanya kuwa vikundi viwili. Kama huwezi vikundi vitakosa kukua. Kama utafanya nusu hizi mbili zinaendelea kukua.

Muda na Vipindi

Masomo ya kipindi kimoja usichukue Zaidi ya saa moja na robo. Kama masomo yataendelea washiriki watachoka na wataacha kuja. Kikundi kinaweza kukutana popote kuanzia juma moja hadi mara moja kwa mwezi. Lazima uwe na kiasi cha mikutano: mara moja kwa muhula, mara kumi n.k.

Viambatanisho

Nyumba. Ni vema kuwa mtu mwingine aongoze kikundi badala ya mwenye nyumba.

Kiongozi. Itazaidi sana kama kiongozi atakuwa ameshiriki katika mafunzo ya Habari Njema (au pengine amesikiliza kanda za mafundisho).

Washiriki. Katika hali nzuri, nusu ya kikundi ni Wakristo na nusu ni wapagani, lakini mtu anaweza kuendesha Masomo ya Habari Njema hata kahali hali sio ya namna hii. Unaweza kualika mtu yeyote kuanzia umri wa miaka 10-100. Isipokuwa jambo moja tu: usialike wale Wakristo ambao ni wazungumzaji sana. Kuna mikutano ya ina nyingine ambayo inawafaa.

Biblia. Kila moja lazima awe na Biblia au nakala ya somo mkononi. Chukua nakala kadhaa kama unafikiri baadhi ya watu watakuja bila Biblia. Chukua toleo ambalo ni rahisi kwa watu ambao sio Wakristo wangependelea.

Mwongozo wa Mafundisho ya Biblia ya Habari Njema.

Mafundisho ya Biblia ya Habri njema yako katika maswali ambayo hayawezi kuwa magumu au rahisi kwa Wakaristo na kwa wasio Wakaristo. Kuna kitabu kimoja ambacho kimeandikwa na Mailis Janatuinen na maswali kwa kila vitabu vinne vyote vya injili (tazama ukrasa wa mwisho).

Kunywa chai nk. Hakikisha kuwa watu wajisikie huru kuondoka baada ya masomo ya Biblia. Kunywa chai iwe kwa wale ambao wana mda. Chakula kitolewe tu kabla ya Kristmas na matukio mengine.

Wakati wa masomo

Kikundi kimekusanyika katika sebuleni ya nyumba ya mtu kwa mara ya kwanza. Utafanya nini?

Kwanza elezea "sharia za mchezo":

1. Katika masomo haya kiongozi hawezi kujibu /maswali yake.
2. Kwa upande mwingine kiongozi hawezi kusema kuwa jibu Fulani ni mbaya.
3. KIongozi arudishe mazungumzo katika kichwa cha somo kama mtu ataanza kuongea mambo mengine nje ya somo.

Washiriki Somo mstari wa Biblia kwa sauti. KIongozi aelezee mazingira ya somo kulingana na kitabu na kuomba ombi fupi. Somo lisomwe kwa kimoyo moyo.

Kiongozi uliza swali moja kwa wakati mmoja na subiri Zaidi ya swali moja. Sawali limewekwa * au swali linategemea laimza lisomwe kama hakuna aliye jibu swali la kwanza.

Kama sheria, kujibu ni kwa hiari. Ni kwa watoto wadogo tu kiongozi anaweza kuuliza kwa kutaja jina.

Hatuandiki ukumbusho katika daftari katika kikundi cha Habari njema.Wala hatuangalii katika mistari mingine ya Biblia Zaidi ya mstari ule ambao tunasoma.

Washiriki wasi angalie maswali wanapojibu. Yanaweza kutolewa kwa kila mtu baada ya masomo au washiriki wanaweza kununua vitabu vyao.

Kama kikundi ni kuzungumzaji, kiongozi aache maswali mengine ili kuweza kumaliza mapema. Hata hhviyo siruke maswali ya miwsho kwa maana hayo ni muhimu sana.

Kam kiongozi ni mwaminifu, wengine watakuwa pia.

Wakati maswali yameisha, kila mmoja anaweza kusema waliyogundua kutoka na somo. Kiongozi anaweza kutoa yak wake.

Mwishowe kiongozi aombe kwa ajili ya shida za washiriki ambazo zilitajwa wakati wa masomo.

Hata kama mtu mmoja tu aliguzwa na upendo wa Yesus, unaweza kusema kuwa somo lilipata mafanikio.

Shida ambazo kiongozi anaweza kukumbana nazo

Unaweza kufanya nini kama hakuna mtu yeyote anaweza kusema chochote?

Shida hii huwa la kawaida wakati wa maswali mawili au matatu ya kwanza katika kikundi kipya. Usibabaike! Watu wataanza kujibu kama wakiongozi hujibu kwa niaba yao. Ni kiogozi tu ambaye anaweza kusikia kuwa kimya kimechukua mda mrefu. Wengine wanafikiri juu ya mistari ya Biblia! Kwa njia hii kimya ni kwa ajili ya manufaa na wala si kinyume.

Kama hakuna yeyote ambaye anaweza kujibu, uliza swali tena mara nyingine.

- Uliza swali kwa njia tofauti.
- Endelea bila majibu kwa swali lingine.

Je utafanya nini kama hujui jibu la swali ambayo mshiriki anauliza?

- Watie moyo washiriki wengine ili waweze kujibu. Mtu mwingine anaweza kujua yale ambayo wewe hujui.
- Ahidi kujibu kipindi kijacho-Na timiza ahadi yako.
- Unaweza kukubaliana kwa urahi kwamba hujui na uendelee.

Utafanya nini kama mtu akitoa jibu ambalo si sahihi?

Usiseme mbele ya mshiriki kwamba hapata kwa maana anaweza kujisikia vibaya.

- Uliza tena wengine. Kwa kawaida mtu mwingine anaweza kutoa jibu sahihi.
- Muulize mtu: "Ni nini katika somo hili ambalo limekufanya ufikirie hivi?" na bila shaka atagundua kwamba somo halisema hayo ambayo alifikiri.

Utafanya nini kama mshiriki akitoka nje ya somo?

Kuna watu ambao hufanya hivi kila mara. Kam akiongozi akiwaruhusu, kutakuwa hakuna mkutano ambao una Yesu kaika kipindi hicho cha masomo.

- Kwa kuweza kuuepuka shida hii unahitaji kusema tangu mwanzo wa somo, "Tutajaribu kumaliza somo hili kwa mda was aa moja. Kama ukiongea mambo mengine nitakurejesha katika somo."
- Kama mtu akiongea kirefu juu ya matukio yake ambayo hayana húhusiano wowote na somo, unaweza kusema, "Ebu na tusikie mazungumzo haya wakati wa chai ebu tupitie maswali yote kwanza."

Utafanya nini kama mtu anajibu kwa kutoa hubiri?

- Kama ukifikiri kuwa hali kama hiyo itatokea, unahitaji kusema katika mwanzo wa somo, "Tafhdhali toa majibu mafunpi ili tuweze kusikia maoni mengi iwezekanavyo.!"

- Endelea na swali linalofuata wakati mtu huyu akipumua.

Urafanya nini kama mtu huyo huyo anajibu kila mara kiasi kwamba wengine hawana nafasi ya kufikiri?

- Sema, "Tafadhali jibu moyo mwako kwanza halafu kwa sauti."
- Usimwangalie mtu huyu.
- Katika kila hali, uliza mawazo ya watu wengine, wakati mtu huyu amemaliza.
- Zungumza naye kwa siri juu ya tatizo hili.

Utafanya nini kama kutatokea kutoelewana kutoka ma mafundisho ya imani?

Hili halitendeki kila mara ila kama litatendeka...

- Summarize both viewpoints.
- Jaribu kufanya pande zote mbili kuangalia somo.
- Ninakubaliana kwamba haukubali na huendelee.
- Kama jambo ni muhimu, basi uliza mchungaji wako afike kipindi kijacho ili kuelezea jambo hilo. La sivyo waruhusu washiriki wasome kitabu au wasikilize kanda juu ya mafundisho ya dini ambayo nahusiaka.

Utafanya nini kama mtu atakatisha masomo ya Biblia kwa kusema kwamba hapende mtindo huu?

Kuna watu ambao hawapendi kupata “jibu sahihi” kwa kila swali, na huwapendi kama mtu mwingine anaonekana kutoa majibu kama hayo.

- Sema, "Tafadhali kaa hadi miwsho wa somo hili. Pengine utaona shabaha ya mtundo huu ilivyo."
- Au unaweza kumwongoza mtu wa namna hii katika mkutano wa kawaida ambapo atasikia hubiri kila mara.

Utafanya nini kama mshiriki mmoja hasemi neno lolote?

Jaribu kuchunguza kama mtu huyu kweli anataka kunyamaza. Wale ambao wanapenda kukaa na bado hawangalii kiongozi. Usiwalazimishe kuongea. Wale ambao wangependa kuongea lakini hawana ujasiri kufanya hivyo humwangalia kiongozi. Unaweza kuwatia moyo waweze kutoa maoni yao mara kwa mara.

Je ikitokea mtu akashirike?

Kama mtu akikashirika Biblia inasema ni chukumu la Mungu na wala sio lako.

- Kiongozi aiondoe kile ambacho kinachukiza katika Biblia. Yesu aliwaruhu wote kijana tajiri na Mfarisayo bila kuwapendeza.
- Jifariji kwamba ni heri kukashirika kuliko kuwa tofauti.

- Ila kama mtu akikashirika kwa mapungufu ya dhambi ya Kanisa au wakristo, basi tukubaliane na tuombe msamaha.

Je ikiwa mshiriki ana shida ya kiakili, ambayo inamfanya kuongea mda wote?

Uzoefu unaonyesha kwamba katika hali hii umtafutie kikundi kingine la sivyo kikundi cha Habari njema hakitadumu.